TANGAZO LA SERIKALI Na. 52 la tarehe 26/1/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA CHALANGWA YA MWAKA 2024

Jina

**1.** Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Katika Eneo la Chalangwa ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji
Sura ya 355

**2.** Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo maalumu la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa Jumla na kina wa eneo

**3.** Mpango wa Jumla na kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

________

JEDWALI

_______

*(Limeandaliwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C1 yenye majira-nukta 564455.9273MS, 9045166.701KZ; baada ya hapo mpaka unelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa 21º33′31″ kwa umbali wa kilomita 4.40 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C2 yenye majira-nukta 562838.1481MS, 9041071.999KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi kwa kufuata uelekeo wa 53º07′55″ kwa umbali wa kilomita 5.46 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C3 yenye majira-nukta 558467.357MS, 9044349.889KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi katika uelekeo wa 16º47′12″kwa umbali wa kilomita 4.50 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C4 yenye majira-nukta 557166.013MS, 9048663.743KZ baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki katika uelekeo wa 64º22′21″ kwa umbali wa kilomita 8.09 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
29 Disemba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*